# RELI NA MATUKIO GAZETI

Toleo la 4, Januari - Desemba 2019

*Toleo Maalum la Mwaka 2019*



# PONGEZI KWA MIAKA MINNE YA UONGOZI



## Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania - TRC wanampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kwa miaka minne ya uongozi.

Shirika linathamini juhudi zilizofanywa na Mhe. Rais kuimarisha Miundombinu ya Reli na kuboresha huduma za usafiri wa reli nchini



Ndg. MASANJA
KUNGU KADOGOSA
MKURUGENZI MKUU TRC

Kwa niaba ya wafanyakazi wenzangu wa Shirika la Reli Tanzania napenda kukushukuru msomaji wa Gazeti hili Maalum la Shirika la Reli Tanzania – TRC linaloelezea Huduma zinazotolewa na Miradi inayosimamiwa na kuratibiwa na TRC kwa lengo la kuelimisha na kuwafahamisha wateja wetu kuhusu mafanikio, changamoto na fursa zilizopo katika Shirika.
Mwaka 2019 umekuwa wa  mafanikio na katika Sekta ya reli nchini tangu kuanzishwa kwake, Shirika limefanikiwa kuendelea kutoa huduma bora za usafiri wa treni za abiria na mizigo, kurejesha safari za treni na mizigo kati ya Dar es Salaam na Kampala na treni za abiria na mizigo Dara es Salaam na Moshi.
Aidha, katika kuboresha huduma Shirika linasimamia mradi wa Uboreshaji wa Reli ya Kati kutoka Dar es Salaam – Isaka umbali wa Kilometa 970 ambao utawezesha reli yetu ya kati kubeba mizigo mingi zaidi na kwenda kasi tofauti na awali.
Nawasihi wananchi waendelee kushirikiana pamoja nasi katika kulinda miundombinu ya reli na kuitunza vyema hasa walio pembezoni mwa njia za reli na kuwa na uelewa ya kwamba miradi yote ya reli inayosimamiwa na shirika kushirikiana na serikali ni miradi yao na inaendelezwa kiufasaha kwa manufaa ya nchi.

BODI YA WAKURUGENZI

JOHN WAJANGA KONDORO
Mwenyekiti wa Bodi
MASANJA KUNGU KADOGOSA
Katibu wa Bodi
WOLFGANG E. SALIA
Mjumbe wa Bodi
EDISON F. MWEYUNGE
Mjumbe wa Bodi
KARIM MATTAKA
Mjumbe wa Bodi
ROGATUS H. MATIVILA
Mjumbe wa Bodi
MAHAMUD MABUYU
Mjumbe wa Bodi
JABIR K. BAKARI
Mjumbe wa Bodi
RUKIA D. SHAMTE
Mjumbe wa Bodi

MENEJIMENTI
FOCUS MAKOYE SAHANI
Kaimu Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Huduma
FAUSTINE KATARAIYA
Kaimu Mkurugenzi wa Ujenzi na Miundombinu ya Reli
FELIX MUTASHOBYA
Kaimu Mkurugenzi wa Ishara, Mawasiliano na Umeme
HENRY MARO MACHOKE
Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Biashara
AMINA MORSAD LUMULI
Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala
EMANUEL BALELE==
Mkurugenzi wa Fedha na Uhasibu
VERONICA SUDAYI
Kaimu Mkurugenzi wa Sheria
MICHAEL SEMAYA
Kaimu Mkurugenzi wa TEHAMA
REGINALD MALELE
Mkuu wa Kitengo cha Ugavi na Manunuzi
DHAHABENI JUMBE
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani
NZEYIMANA DYEGULA
Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji
JAMILA MBAROUK
Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano
MAIZO MGEDZI
Mkuu wa Kitengo cha Usalama wa njia ya Reli
PETER MATHEW
Mganga Mkuu Hospitali ya Reli
PIUS KABEREGE
Kaimu Mkuu wa Chuo cha Reli Tanzania

# 01|Yaliyomo


*Kuanza kwa Safari za treni za abiria Dar - Moshi*

*Miundombinu ya Umeme yaanza kujengwa katika mradi wa SGR Dar - Morogoro*

*Waziri Mkuu afanya ufunguzi reli ya Tanga - Moshi*

*Hafla ya uzinduzi wa Uchomeleaji wa Reli ya Kisasa*

*Uchorongaji wa Handaki refu zaidi nchini wakamilika*

*Maadhimisho ya mwaka mmoja wa mafanikio usafiri wa reli Dar - Kampala*

*Picha za Matukio tofauti*

*Matangazo na Ratiba za treni*

*Ziara ya Rais wa Congo na ziara ya Waziri wa Sudani Kusini kuona maendeleo ya Mradi wa SGR*

*Viongozi wa Jumuiya ya Wazazi CCM watembelea Mradi wa SGR*

*UVCCM C hamwino watembelea Mradi wa SGR*

*Rais wa Benki ya Maendeleo ya Biashara Kusini na Mashariki mwa Afrika atembelea Mradi wa SGR*

*Mawaziri wa Mambo ya Nje nchi za Afrika na Nordic watembelea Mradi wa SGR*

*Miaka minne ya mafanikio ya serikali ya awamu ya Tano*

*Picha na Matukio*

*Safari ya Kampuni ya Wasafi Classic Baby kwa kutumia Treni ya Kisasa ya Deluxe*

*Mahojiano na Wadau*

*Maoni wa Wadau*

*Ukarabati wa Mabehewa kuwa chachu ya Ukuaji uchumi nchini  kupitia usafirishaji mizigo*

*Makala ya Afya*

*Neno la Shukurani*

Na Mwandishi wetu TRC



## TRC YAANZA KUTOA HUDUMA YA TRENI ZA ABIRIA KATI YA DAR ES SALAAM NA MOSHI

Shirika la Reli Tanzania - TRC laanza kutoa huduma ya usafiri wa treni za abiria iliyokuwa imesimama kwa zaidi ya miaka 25 kati ya Dar es Salaam na Moshi, safari hiyo imeanza rasmi katika stesheni ya Kamata jijini Dar es Salaam hivi karibuni Desemba, 2019.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini - LATRA Mhandisi Dkt. John Ndunguru ameshuhudia kuanza kwa huduma hiyo mara baada ya kujiridhisha kufuatia majaribio ya treni kupita katika reli ya kaskazini hivi karibuni Desemba 01, 2019 kuanzia Dar es Salaam hadi Moshi mkoani Kilimanjaro.

Aidha, wananchi wameonesha kuipokea huduma ya usafri wa treni Dar - Moshi kwa furaha ambapo Shirika kwa sasa litakuwa likifanya safari ya treni ya kisasa ya Deluxe mara tatu kwa wiki katika siku za Jumatatu, Jumatano na Ijumaa kutoka Dar es Salaam na Jumanne, Alhamis na Jumamosi kutoka Moshi mkoani Kilimanjaro.

Katika hafla hiyo Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Dkt. John Ndunguru amewaomba abiria wote ambao wasafiri na treni ya Deluxe kuwa mabalozi wazuri kuitangaza treni hiyo, pia amewataka wananchi kuendelea kutunza na kulinda miundombinu ya reli kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Huduma Shirika la Reli Tanzania Ndugu Focus Sahani amewashukuru wananchi walioamua kusafiri na treni ya Deluxe kwa kuwa wanaunga mkono jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli za kurejesha huduma za usafiri katika maeneo ambayo huduma hizo zilisitishwa kwa muda mrefu.

Hata hivyo treni hiyo ilipokelewa rasmi na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TRC Prof. John Kondoro na wananchi ilipowasili katika Stesheni ya Moshi Desemba 7, 2019.

Shirika linatoa rai kwa watanzania kuendelea kulinda miundombinu ya reli ili kuokoa fedha za serikali kwa kuwa reli hii imekarabatiwa kwa fedha za watanzania, hivyo mtanzania anayehujumu miundombinu ya reli analihujumu taifa lake mwenyewe. Endapo utaona vitendo vyovyote vya kihalifu katika miundombinu ya reli tafadhali ripoti katika vyombo vya usalama au piga simu ya bure 0800110042 .

### TAARIFA KWA UMMA

KUONGEZEKA KWA SIKU ZA SAFARI ZA TRENI YA ABIRIA DAR ES SALAAM – KILIMANJARO

Dar es Salaam, Desemba 12, 2019

Shirika la Reli Tanzania - TRC linawatangazia wateja wanaotumia huduma ya usafiri wa reli nchini, kuongezeka kwa idadi ya siku za safari kwa treni ya abiria kutoka Dar es Salaam kuelekea Moshi mkoani Kilimanjaro, Kutokana na maombi ya uhitaji wa wateja juu ya usafiri wa treni ya abiria kuanzia siku ya Jumatatu Desemba 16, 2019.

Awali treni ya abiria ilikuwa ikifanya safari kati ya Dar es Salaam na Moshi tangu tarehe 6.12.2019 mara nne kwa wiki, ambapo ilikuwa ikitoka Dar es Salaam siku ya Jumanne na Ijumaa, na kutoka Moshi siku ya Jumamosi na Jumatano. Shirika limefanyia kazi maombi ya wateja kwa kuongeza idadi ya safari za treni kuwa mara sita kwa wiki.

Treni ya abiria itakua ikianza safari kutoka Dar es Salaam kwenda Moshi siku za Jumatatu, Jumatano na Ijumaa Saa 10:30 Alasiri na kutoka Moshi kuelekea Dar es Salaam siku za Jumanne, Alhamisi, na Jumamosi Saa 10:30 Alasiri.

Shirika linawashukuru wateja kwa kuonesha kufurahia huduma za usafiri wa treni ya abiria mkoani Kilimanjaro ambao ulisimama kwa takribani miaka 26 na kuonesha ushirikiano katika kipindi cha ukarabati wa miundombinu ya reli Daresasalam – Moshi.

Sambamba na hilo Shirika linawaomba wananchi kuendelea kutoa ushirikiano ili kuhakikisha miundombinu ya reli inakuwa salama muda wote ili kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji nchini

**Imeandaliwa na Mkuu wa kitengo cha Uhusiano TRC**

## MIUNDOMBINU YA UMEME YAANZA KUJENGWA KATIKA MRADI WA SGR DAR - MOROGORO

Na Mwandishi wetu TRC



*Sehemu ya Reli ya Kisasa - SGR ikiwa imewekwa nyaya za umeme kwa ajili ya uendeshaji wa treni za reli ya kisasa zitakazotumia umeme, eneo la Soga Kibaha mkoani Pwani.*




*Mafundi wa kampuni ya Yapi Merkezi wakiendelea na kazi ya uwekaji nyaya za umeme kwa ajili ya umeme utakaotumika katika treni za SGR, Soga mkoani Pwani*

Miundombinu ya Umeme kwa ajili ya kusafirisha umeme kutoka kwenye chanzo pamoja na miundombinu mingine ya kupokea umeme utakaotumika kuendesha treni za Reli ya Kisasa - SGR yaendelea kujengwa hivi karibuni Novemba 2019.

Miundombinu hiyo ni pamoja na nguzo za umeme zitakazosafirisha umeme kutoka katika chanzo cha umeme cha Kinyerezi na kuleta katika vituo maalum vilivyopo pembezoni mwa reli ya kisasa ambazo kwa kitaalamu zinaitwa *'electrick transmisiion tower'*.

Kwa kipande cha Dar es Salaam Morogoro jumla ya nguzo 445 za umeme zinajengwa na Mkandarasi L and T kutoka India ambapo hivi sasa ujenzi wake umefikia zaidi ya asilimia 62.



*Moja kati ya vituo vinne vya kuhifadhi umeme utakaotumika katika treni za kisasa za SGR kinachojengwa eneo la Soga mkoani Pwani.*

Aidha umeme utakaokuwa unatumika kuendesha treni za reli ya kisasa utatoka katika chanzo cha umeme cha Kinyerezi ambapo chanzo hiko hakitakuwa na matumizi mengine yoyote isipokuwa kitakuwa maalum kwa kuzalisha umeme kwa ajili ya kuendesha treni pekee.

Katika Miunbombinu ya Reli ya Kisasa vinajengwa vituo vinne vya umeme ambavyo vitakuwa vinapokea umeme kutoka nguzo kubwa, na kuupoza kisha kuusafirisha katika nguzo maalum zinazojengwa pembezoni mwa reli umbali wa Mita 50 kutoka nguzo moja.

Nguzo hizo ndizo zitakazobeba nyaya ambazo zitapeleka nishati ya umeme kwenye injini za treni kwa jili ya kuendesha treni hizo, ujenzi wa nguzo hivi unaendelea ambapo jumla ya nguzo 4060 zinasimikwa kuanzia Dar es Salaam hadi Morogoro.



*Muonekano wa Nguzo za umeme wa Reli ya Kisasa - SGR zitakazokuwa zinasafirisha umeme kutoka kwenye chano kwenda katika vituo vya vya kupoza umeme kwa ajili ya kutoa nishati ya kuendesha treni.*

Sifa kuu ya nguzo hizi ni kuwa zina urefu wa Mita 9.5 kila moja huku uzito wa nguzo moja ukiwa wa Tani 2.4, pia zina uwezo wa kudumu kwa zaidi ya miaka 120 na kutokana na madini ya Zinki yaliyowekwa katika nguzo hizo kwa ajili ya kuzuia kutu.

Sambamba na ujenzi wa miundombinu hiyo Shirika la Reli Tanzania kwa kushirkiana na Shirika la usambazaji Umeme nchini limeendesha zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yametwaliwa ili kupisha ujenzi wa miundombinu hiyo kipande cha Dar es Salaam - Morogoro

Zoezi limeendeshwa na Maafisa kutoka Shirika la Reli Tanzania, Shirika la Usambazaji Umeme nchini - TANESCO, Chuo Kikuu cha Ardhi na viongozi wa serikali za mitaa na vijiji husika katika kijiji cha Mtego wa Simba, Kinonko, Kidugalo, Mikese, Sinyaulimbe, Ngerengere, Mgude, Mhungamkola na mtaa wa Pangawe.

Mradi huu utakapokamilika Tanzania itakuwa nchi ya kwanza kuwa na treni zinazotumia umeme na zinazobeba mzigo wa Tani 10,000 kwa mkupuo kwa mwendokasi usiopungua Kilometa 120 kwa saa.

# MRADI WA UBORESHEJI WA RELI YA KATI – TIRP DAR ES SALAAM – ISAKA WASHIKA KASI



Na Mwandishi wetu TRC

Serikali ya awamu Tano inayoongozwa na Rais Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli inaendelea kuhakikisha kwamba, Tanzania inaimalika katika Sekta ya uchukuzi na usafirishaji kwa kuboresha miundombinu ya reli nchini. katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/19,

Serikali imetenga jumla ya Shilingi bilioni 252.6 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya reli kupitia Mfuko wa Reli haya yote yanafanyika Ili kuimarisha miundombinu katika sekta ya usafirishaji wa reli nchini kwa masilahi ya Taifa.

Shirika la Reli Tanzania – TRC linaendelea na usimamizi na kutekeleza wa mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya reli nchini Ili kuongeza ufanisi katika utendaji na usafirisha wa mizigo na abiria.

Serikali inaendelea kutoa kipaumbele katika uwekezaji wa miundombinu wezeshi ya kiuchumi katika usafirishaji ambapo kwa sasa inaendelea na mradi wa uboreshaji wa reli ya kati - TIRP Dar es Salaam mpaka Isaka, Kahama Mkoani Shinyanga umbali wa kilomita 970, chini ya mkandarasi China Civil Engineering and Construction Corporation – CCECC.

Serikali kupitia Shirika la Reli nchini liliamua kuboresha reli ya 'Meter Gauge' baada ya kupungua ufanisi katika utendaji kwani reli hiyo imedumu kwa zaidi ya miaka 100 tangu ilipojengwa wakati wa ukoloni hivyo kupelekea miundombinu hiyo kuchakaa.

Lengo la maboresho haya ni kuiwezesha reli ya zamani kutoa huduma ya usafiri wa abiria na mi zigo kwa ufanisi na uhakika. Mradi huo unagharimu pesa za kimarekani dola millioni 300 ambapo uboreshaji wake umefikia zaidi ya asilimia 71 tangu kuanza utekelezaji wake mwezi Juni 2018. Mradi huo unahusisha uboreshaji wa miundombinu ya reli ikiwemo Makalavati, tuta la reli, Madaraja makubwa na madogo na kuweka mifumo ya kisasa ya mawasiliano.

Kazi mbalimbali zinaendelea kufanyika ni kuimarisha tuta kwa kuondoa kokoto za zamani na kuweka kokoto mpya, kuimarisha Makalavati, Madaraja makubwa na madogo, lakini pia kuiunganisha reli kwa kutumia mashine ya 'Mobile Flash Butt plant' na kuifanya reli kuwa moja (contionus welded rail).

Matokeo makubwa yataanza mara tu baada ya kukamilika zoezi la uboreshaji ambapo ufanisi katika mwendokasi wa treni utaongezeka ambapo treni za abiria na mizigo zitatembea kwa mwendokasi hadi Kilometa 75 kwa saa tofauti na sasa ambapo treni zilnakwenda Kilometa 30 - 35 kwa saa, hii itasaidia kupunguza muda wa safari na kusaidia kuendelea kwa kasi kwa shughuli nyingine za kiuchumi.

Aidha kwa upande wa uwezo wa treni kubeba mzigo mkubwa utaongezeka pia, treni itakuwa na uwezo wa kubeba mizigo kutoka tani 14 – 18.5, abiria nao watasafiri kwa starehe bila kuwepo na mtikisiko wa mara kwa mara kwani reli itakuwa imeungwa katika maungio yake.

Wakati Shirika likiendelea na utekelezaji wa uboreshaji wa reli ambayo ni chachu ya maendeleo ya watanzania, Shirika la reli nchini likaamua kufanya kampeni ya uwelewa kwa wananchi wa Tanzania kuhusu faida za miradi sambamba na ulinzi na usalama wa wananchi na miundombinu ya reli ambayo ni faida kwa watanzania na kizazi cha baadae.

Kampeni hiyo ilifanyika katika maeneo ya maeneo yaliyopitiwa na reli ikilenga kuwaeleimisha watanzania kuhusu faida watakazopata wakati wa ujenzi na baada ya miradi hii kukamilika, umuhimu wa kuzingatia na kulinda miundombinu ya reli, matumizi ya alama za reli kwa usalama wa wananchi, kutoa elimu juu ya fursa zinazoambatana na ujenzi wa reli, kusikiliza kero za wanachi na wafanyakazi, utunzaji wa mazingira wakati wa ujenzi lakini pia Shirika lilitoa mfumo mpya ambao wananchi watatumia kutoa maoni, changamoto na kero ambazo wanakutana nazo wakati utekelezaji wa uboreshaji ukiendelea.

## RAIS MAGUFULI NA RAIS MUSEVENI WATEMBELEA BANDA LA TRC KATIKA KONGAMANO LA BIASHARA KATI YA TANZANIA NA UGANDA



Na Mwandishi wetu TRC

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli na Rais Yoweri Kaguta Museveni wa Uganda watembelea banda la Reli Tanzania - TRC na kujionea huduma na Miradi inayosimamiwa na TRC katika siku ya ufunguzi wa kongamano la kwanza la biashara kati ya Tanzania na Uganda katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha J.K Nyerere jijini Dar es Salam hivi karibuni Septemba, 2019.

*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. John Pombe Magufuli akipata Maelezo kuhusu maendeleo ya Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa alipotembelea Banda la TRC katika maonesho ya SADC katika kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha J.K Nyerere.*

## HAFLA YA UZINDUZI WA UCHOMELEAJI WA RELI YA KISASA




*Waziri wa Ujeni Uchukuzi na Mawasiliano mhandisi Isack Kamwelwe akitazama sehemu ya reli ambayo imeungwa kwa kuchomelewa.*

Waziri wa ujenzi uchukuzi na mawasiliano Mhandisi Isack Kamwelwe afungua rasmi kazi ya kuunganisha Reli ya kisasa - SGR nje kidogo ya kambi ya SGR ya Soga Kibaha Aprili 2019.

Mhe. Waziri Kamwelwe azindua rasmi kazi ya kuchomea Reli ya kisasa - SGR kwa lengo la kuunganisha na kuondoa maungio yote kwenye Reli.

Aidha Waziri Kamwelwe aliongezea kuwa Ujenzi wa reli ya SGR unakwenda vizuri kwa kuwa kazi inaonekana na inakwenda kwa kasi nzuri.

Amesema Waziri Kamwelwe "kama mnavyoona vifaa viko hapa tumefikia hatua ambayo inaonekana, tuta limeshajengwa, mataruma yamewekwa na reli imewekwa, leo nimezindua kuunganisha reli kwa umeme bila kutumia 'material' mengine yoyote, uungaji huu umefanyika mara ya kwanza Tanzania, reli hii itakuwa ni moja kutoka Dar es Salaam mpaka Makutupora"

Waziri Kamwelwe ameongeza kuwa serikali imewapa kipaumbele wahandisi na mafundi wazawa katika mradi pamoja na kuendesha mafunzo ndani na nje ya nchi ili kuhakikisha kuwa kuna wataalam wa kutosha.

Hafla ilihudhuriwa na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa, Wafanyakazi TRC, wanahabari pamoja na wananchi wa Soga Kibaha mkoani Pwani

## WAZIRI MKUU MHE. KASSIM MAJALIWA AFANYA UFUNGUZI WA RELI YA TANGA - MOSHI

Na Mwandishi wetu TRC



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa, Katibu wa Itikadi na Uenezi CCM Ndugu Humphrey Polepole pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa wakifurahia kuipokea treni ya kwanza ya mizigo ilipowasili stesheni ya Moshi Julai 2019.*

Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe . Kassim Majaliwa amefanya ufunguzi wa njia ya reli ya Tanga mpaka Moshi/Kilimanjaro katika hafla iliyofanyika mjini Moshi , Kilimanjaro hivi karibuni Julai 2019, iliyohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, wa vyama pamoja na wa dini.

Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa amelipongeza Shirika la Reli Tanzania -TRC kwa Kurejesha njia ya Tanga-Moshi ambayo takribani miaka 12 ilikuwa haifanyi kazi. Waziri Mkuu amesema kuwa mafanikio haya ni utekelezaji wa sera ya kitaifa na Mkakati wa Nchi kuinua sekta mbalimbali za kimkakati ili inchi ya Tanzania ifikie Uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Waziri mkuu aliongeza kuwa juhudi na kujitoa kulikofanyika kurejesha njia ya reli kuanzia Dar es Salaam hadi Tanga na kisha kuelekea Moshi ,Kilimanjaro ni uamuzi wa busara uliokuja kwa wakati na unaoshamirisha azima yetu ya kuchochea ukuaji wa uchumi lakini na kuyabadili maisha ya wananchi kupitia huduma bora za usafiri na uchukuzi "Kamwe hatuwezi kufikia hadhi hiyo muhimu kiuchumi bila kuwa na miundombinu imara ikiwemo ya reli" alisema Mhe. Kassim Majaliwa.

Aidha Waziri Mkuu amebainisha kuwa Tanzania inapakana na nchi zaidi ya tano ambazo zinategemea sana miundombinu ya nchi ya Tanzania ya usafirishaji na uchukuzi ndani ya nchi ili kupitisha bidhaa. Pia aligusia juu ya mradi mkubwa wa kihistoria wa SGR unaoendelea kuanzia Dar es Salaam hadi Mokutopola na kusema kuwa Serikali ya awamu ya tano imewekeza takribani Shilingi Bilioni 7.2 fedha za walipa kodi kutekeleza mradi huo.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano Mhe. Atashasta Nditiye ameipongeza Serikali ya awamu ya tano kwa kutoa fedha pia amepongeza bodi na uongozi wa Shirika la Reli Tanzania katika ufuatiliaji na utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya ufufuaji wa Shirika na njia mbalimbali za reli zilizokufa kwa miaka mingi hapa nchini. Hata hivyo Naibu Waziri ametoa rai kwa wafanyakazi wa TRC na watanzania kuwa walinzi wa miundombinu ya reli ambayo ni kichocheo kikubwa cha uchumi nchini



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa, na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli n Tanzania wakifurhia mara baada ya kupokea treni ya kwanza ya mizigo katika stesheni ya Moshi mkoani Kilimanjaro hivi karibuni Julai 2019.*

## UCHORONGAJI WA HANDAKI REFU ZAIDI TANZANIA WAKAMILIKA KILOSA MKOANI MOROGORO

Na Mwandishi wetu TRC

Ujenzi wa awamu ya pili ya Reli ya Kisasa – SGR kipande cha kutoka Morogoro hadi Makutupora Mkoani Singida umefika zaidi ya asilimia 22, huku kazi ya kuandaa tuta, vivuko na madaraja ikiendelea lakini kubwa zaidi ni uchorongaji wa mahandaki manne yatakayopitisha treni ya umeme.

Kupitia mradi wa SGR Tanzania itaandika historia nyingine Wilayani Kilosa Mkoani Morogoro ambapo ujenzi wa Mahandaki manne likiwemo handaki moja refu zaidi lenye urefu wa kilometa 1.031 ukifanywa na 95% ya wahandisi watanzania kwa kutumia fedha za watanzania walipa kodi. Hivi sasa uchorongaji wa mlima kwa ajili ya handaki namba 2 ambalo ni refu zaidi nchini umekalika kwa asilimia 100, zoezi la kukamilisha uchorongaji wa handaki namba 2 kwa upande wa kuingilia na upande wa kutokea limefanyika usiku wa tarehe 5 Desemba 2019, ambapo zoezi hilo ambalo lilianza tarehe 22 Julai, 2019 na kuchukua jumla ya siku 137 kukamilika.

Mahandaki mengine matatu (Handaki namba moja – mita 424, Handaki namba tatu – mita 318 na Handaki namba nne – mita 847) yenye jumla ya wa Mita 1589 yanaendelea hayo yanajengwa ili kuepuka athari za mto Mkondoa ambao umekuwa ukifurika kipindi cha mvua kubwa na kuathiri miundombinu ya reli ya zamani hivyo basi kutokana na jografia ya wilaya ya Kilosa sambamba na athari za mvua ambazo hupelekea kufurika kwa mto Mkondoa na kuathiri miundombinu ya reli mkandarasi akajenga mahandaki ambayo yatazuia athari za mafuriko wakati wa mvua.

Mhandisi Amiri Khamis, Mkaguzi wa mahandaki kutoka kampuni ya KORAIL JOINT VENTURE ambao ni washauri wa ujenzi wa mradi wa SGR amebainisha kuwa kazi ya uchorongaji mlima kwa ajili ya ujenzi wa handaki namba mbili lenye urefu wa KM 1.031 imekwisha, hata hivyo mhandisi ametoa pongezi za dhati kwa Mkandarasi YAPI MARKEZI, KORAIL JOINT VENTURE NA TRC kwa juhudi, ushauri na ushirikiano waliouonesha wakati wa shughuli nzima ya utoboaji handaki na kukamilika kwa wakati.







## TRC, WFP, URC, TPA NA MSCL WAADHIMISHA MWAKA MMOJA WA MAFANIKIO



Shirika la Reli Tanzania – TRC, Shirika la Mpango wa Chakula Duniani – WFP, Mamlaka ya Bandari Tanzania – TPA, Shirika la Reli Uganda – URC pamoja na Kampuni ya Huduma za Meli Tanzania – MSCL waadhimisha mwaka mmoja wa mafanikio katika usafirishaji wa Mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam, Mwanza hadi Portbell nchini Uganda kupitia Ziwa Victoria hivi Karibuni Julai 2019.

Usafiri wa reli kutoka Bandari ya Dar es salaam hadi Portbell nchini Uganda kupitia reli ya kati kwa ushirikiano wa TRC, TPA, MSCL, URC na WFP umezidi kuimarika tangu kurejeshwa kwa safari hizo mwezi Julai 2018 ambapo Shirika la Mpango wa Chakula Duniani limesafirisha jumla ya Tani 36,000 hadi kufikia mwezi Julai 2019.

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhandisi Isack Kamwelwe amethibisha hilo alipokuwa akihutubia hafla fupi ya kuadhimisha mwaka mmoja wa mafanikio hayo katika Bandari ya Mwanza Kusini jijini Mwanza kabla ya kuanza kwa safari ya 14 ya Meli ya MV Umoja inayobeba shehena ya Chakula pamoja na Mizigo mingine kuelekea Portbel nchini Uganda na hatimaye hadi Sudani Kusini.

Hafla ilihudhuriwa na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhe. Isack Kamwelwe, Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Innocent Bashungwa, Katibu Mkuu Sekta ya Uchukuzi Dkt. Leonard Chamuriho, Wakuu wa Mikoa ya Geita na Mwanza, Mkurugenzi Mkuu TRC Ndugu Masanja Kadogosa, Mkurugenzi Mkuu TPA Mhandisi Deusdedith Kakoko, Mwakilishi Mkaazi WFP Bwana Michael Danford, Kaimu Mkurugenzi wa MCSL Mhandisi , wafanyakazi, viongozi wa chama na serikali, wanahabari pamoja na wananchi.

Akizungumza katika hafla hiyo Waziri Kamwelwe anesema kuwa`usafiri wa reli na meli ni nafuu zaidi kuliko aina nyingine za usafiri

"Tafiti zimebainisha kuwa usafirishaji kwa njia ya reli na meli ni usafiri wa uhakika na wenye gharama nafuu hususani kwa mizigo inayokwenda umbali mrefu ukilinganisha na aina nyingine za usafiri, mfano takwimu za WFP zinaonesha kuwa gharama za usafirishaji zimepunguza kwa 40% kwa kutumia njia hizi za usafiri" Alisema Waziri Kamwelwe

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kadogosa amesema lengo kuu la safari hii ni kuutangaza ushoroba wa kati kwa kwa kuwa njia hiyo inaokoa muda na gharama za usafirishaji

"Unapotumia reli unakuwa na nafasi nzuri ya kupanga bei ya bidhaa kwa unafuu, pia kwa kutumia njia hii mfanyabiashara atapunguza zaidi ya siku nne kusafirisha mzigo hadi Uganda" alisema Kadogosa

Hafla hiyo iliambatana na safari kuanzia Bandari ya Mwanza Kusini hadi Bandari ya Portbell na kupokelewa na wenyeji ambao ni

Waziri wa Uchukuzi nchini Uganda Mhe. Edward Katumba Wamala na Maafisa wa Shirika la Reli Uganda ambapo timu ya maafisa wa URL, TRC, WFP, TPA na MSCL walipata fursa ya kutembelea Bandari ya Jinja nchini Uganda kwa lengo la kuendelea kuimarisha huduma za usafiri wa reli kutoka Mwanza hadi Bandari ya Jinja kwa kuifufua bandari hiyo pamoja na miundombinu ya reli ili kufungua safari za Mizigo kutoka Mwanza hadi Jinja.

Akizungumza na TRC Reli TV Charles Ruzigye Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Meli Shirika la Reli Uganda amesema kuwa URC kwa kushirikiana na TRC, TPA, MSCL na WFP tumepanga kurudisha huduma ya usafiri kutoka Mwanza hadi Jinja kwa kufungua njia ya reli ya pamoja na Bandari ya Jinja.

"Mpango ni kupanua bandari pamoja na kukarabati reli kutoka Bandari ya Jinja hadi kwenye sehemu ya kuweka mizigo (Yard) na kuhakikisha kuwa kwa kushirikiana na wenzetu baada ya miezi mitatu hadi minne njia hii inaanza kufanya kazi" alisema Bwana Ruzigye

Mkuu wa Usafirishaji WFP Tanzania Ndugu Mahmudu Mabuyu amesema kuwa kufunguliwa kwa njia na Bandari ya Jinja kutasaidia kusafirisha kwa urahisi mizigo ya WFP pamoja wafanyabiashara wa Tanzania na Uganda .

Na Mpiga Picha Wetu TRC



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe, Dkt. John Pombe Magufuli akipata ufafanuzi kuhusu Maendeleo ya Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa alipotembelea banda la TRC katika Maonesho ya 4 ya Viwanda na Biashara ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika - SADC katika ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa J.K Nyerere jijini Dar es Salaam Agosti 2019

*Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano Shirika la Reli Tanzania - TRC Bi Jamila Mbarouk akifafanua jambo kwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Dkt. Mohammed Ally Shein alipotembelea banda la TRC katika Maonesho ya 4 ya Viwanda na Biashara ya Jumuiya ya Nchi a Kusini mwa Afrika - SADC katika ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Mwalimu J.K Nyerere jijini Dar es Salaam Agosti 2019.*



Na Mpiga Picha Wetu TRC



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akipata maelezo kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR kutoka kwa Meneja Mradi wa SGR kipande cha Dar es Salaam - Morogoro Mhandisi Machibya Masanja, Soga kihana mkoani Pwani.



Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano Shirika la Reli Tanzania - TRC Bi Jamila Mbarouk akifafanua jambo kwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa alipotembelea banda la TRC katika Maonesho ya 4 ya Viwanda na Biashara ya Jumuiya ya Nchi a Kusini mwa Afrika - SADC katika ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Mwalimu J.K Nyerere jijini Dar es Salaam Agosti 2019.

Na Mpiga Picha Wetu TRC




*Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa (kulia) akikabidhi hundi ya Shilingi Bilioni Moja kwa Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Philip Mpango jijini Dodoma hivi karibuni Novemba, 2019.*



*Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa (kushoto akiwaelezea Mawaziri wa Mambo ya nje kutoka nchi za Nordic na Afrika kuhusu maendeleo ya Mradi wa SGR Dar es Salaam - Morogoro walipofanya ziara kuona maendeleo ya mradi Vingunguti jijini Dar es Salaam hivi karibuni Novemba, 2019.*



*Kaimu Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Huduma zitolewazo na Shirika la Reli Tanzania Bwana Focus Makoye Sahani (kulia) akimuelezea Mtangazaji wa Shirika la Utangazaji nchini Bwana Amini Mgeni kuhusu mafanikio ya Shirika katika kuboresha huduma za usafiri wa reli nchini kwa kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, Kamata jijini Dar es Salaam hivi kaibuni Novemba, 2019.*

# PICHA; MATUKIO TOFAUTI WAKATI WA MAADHIMISHO YA WIKI YA SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Na Mpiga Picha Wetu TRC




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa akielezea miaka minne ya Rais Magufuli katika sekta ya reli alipofanya mkutano na waandishi wa habari katika ukumbi wa mikutano habari maelezo jengo la Kumbi za Mikutano JNICC Dar es Salaam hivi karibuni Desemba 2019.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa akiwa katika studio za clous media kwenye kipindi cha 360 kuelezea mafanikio ya sekta ya reli katika kipindi cha miaka minne ya uongozi ya awamu ya tano chini ya Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli Desemba 2019



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa (kulia) akielezea kuhusu kuongezeka siku za afari za treni ya Deluxe Dar - Moshi ambapo safari hizo zimeongezwa kutoka mara nne hadi sita kwa wiki alipohojiwa na Mtangazaji wa Kipindi cha Morning Trumpet Jamal Hashim katika kituo cha Azam TV Dar es Salaam hivi karibuni Desemba 2019



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa (aliyevalia suti ya buluu) akiwa katika picha ya pamoja na Maafisa Uhusiano na Habari wa Shirika wakiongozwa na Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano TRC Bi. Jamila Mbarouk pamoja na Mtangazaji wa kipindi cha Morning Trumpet katika Studio za Azam TV Desemba, 2019.



Meneja Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Mhandisi Machibya Masanja akielezea mikakati ya ujenzi wa reli za mijini katika jiji la Dar es Salam na Dodoma katika Stduio za Magic FM Dar es Salaam Desemba, 2019.



Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Biashara Bwana Henry Machoke akielezea mikakati ya Shirika katika kuhakikisha huduma za usafiri wa treni Dar - Moshi unakuwa wa kudumu ili kupunguza adha ya usafiri kwa wananchi hususani katika kipindi cha mwisho wa

Na Mpiga Picha Wetu TRC

## PICHA ZIKIONESHA SHUGHULI ZINAZOENDELEA KATIKA MRADI WA SGR DAR ES SALAAM - MOROGORO



*Rais wa Benki ya Maendeleo ya Biashara Mashariki na Kusini mwa Afrika Dkt. Admass Tadesse (kulia) akipata maeleo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la ReliTanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa kuhusu maendeleo ya Ujenzi wa Stesheni ya Kisasa jijini Dar es Salaam hivi karibuni Novemba, 2019.*



*Meneja Mradi wa Reli ya Kisasa - SGR Dar es Salaam - Morogoro Mhandisi Machibya Masanja (kati) akimuelezea Rais wa Benki ya Maendeleo ya Biashara Mashariki na Kusini mwa Afika Dkt. Admass Tadesse kuhusu ubora wa Mataruma yanayotumika katika ujenzi wa reli ya SGR Vingunguti Dar es Salaam hivi karibuni Novemba 2019.*




*Mafundi wakiendelea na kazi ya kutandaza nyaya katika nguzo za umeme wa Reli ya Kisasa - SGR kipande cha Dar es Salam - Morogoro katika eneo la Soga Kibaha mkoani Pwani hivi karibuni Novemba 2019.*



*Maafisa wa Shirika la Reli Tanzania pamoja na Mtendaji wa kijiji cha Mikese Mjini wakihudumia wananchi wakati wa zoezi la kukabidhi hundi za malipo ya fidia ili kupisha ujenzi wa miundombinu ya umeme wa reli ya kisasa - SGR mkoani Morogoro hivi karibuni Novemba 2019.*





*Muonekano wa Nguzo za umeme wa Reli ya Kisasa - SGR zitakazokuwa zinasafirisha umeme kutoka kwenye chanzo kwenda katika vituo vya kupoza umeme kwa ajili ya kutoa nishati ya kuendesha treni.*

Na Mpiga Picha Wetu TRC

## PICHA ZIKIONESHA MAENDELEO YA MRADI WA RELI YA KISASA DAR ES SALAAM - MAKUTUPORA




*Muonekano wa moja kati ya Stesheni ndogo nne za reli ya kisasa zinazojengwa kati ya Dar es Salaam na Morogoro.*




*Ujuenzi wa Stesheni kubwa ya reli ya kisasa ikiendelea eneo la Stesheni jijini Dar es Salaam.*




*Muonekano wa Daraja lenye urefu wa Kilometa 2.5 linalojengwa kuanzia Stesheni hadi Ilala jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kupitisha treni za kisasa.*



*Kazi ya ujenzi wa Daraja kwa ajili ya kupitisha reli ya kisasa - SGR katika mto Ruvu ikiendelea.*

## PICHA ZIKIONESHA MAENDELEO YA MRADI WA UBORESHAJI WA RELI YA KATI DAR ES SALAAM - ISAKA



*Mtaalamu akiendele na kazi ya kuunganisha reli kwa mtambo maalum kuchomelea reli.*



*Mafundi wakiendelea na kazi ya kuondoa vifungashio katika reli ili kuwaweze-sha wataalamu kuendelea na kazi ya kuchomelea reli*



## Twenzetu Kilimanjaro na Treni ya Deluxe kila Jumatatu, Jumatano, Ijumaa

Kata tiketi yako katika Stesheni zifuatazo
KAMATA DAR ES SALAAM
RUVU | WAMI | MKALAMO
GENDAGENDA | MNYUSI
KOROGWE | MOMBO | MKOMAZI
HEDARU | MAKANYA | SAME
KISANGIRO | KAHE | MOSHI

***SAFIRI NASI KWA GHARAMA NAFUU***

**NAULI ZA TRENI YA DELUXE KUTOKA DAR KUELEKEA MOSHI**

| KITUO | KM | MADARAJA YA NAULI | | |
|---|---|---|---|---|
| | | DARAJA LA TATU | DARAJA LA PILI KUKAA | DARAJA LA PILI KULALA |
| WAMI | 151 | 7,600 | 10,800 | 18,000 |
| MKALAMO | 203 | 8,900 | 12,700 | 21,200 |
| GENDAGENDA | 230 | 9,400 | 13,400 | 22,200 |
| MNYUSI | 276 | 10,300 | 14,600 | 24,300 |
| KOROGWE | 291 | 10,700 | 15,300 | 25,400 |
| MOMBO | 335 | 11,600 | 16,500 | 27,500 |
| MKOMAZI | 374 | 12,500 | 17,800 | 29,600 |
| HEDARU | 406 | 13,400 | 19,100 | 31,700 |
| MAKANYA | 425 | 13,800 | 19,700 | 32,800 |
| SAME | 459 | 14,200 | 20,300 | 33,800 |
| KISANGIRO | 518 | 15,600 | 22,200 | 37,000 |
| KAHE | 538 | 16,000 | 22,900 | 38,100 |
| MOSHI | 558 | 16,500 | 23,500 | 39,100 |

**NAULI ZA TRENI YA DELUXE KUTOKA MOSHI KUELEKEA DAR**

| KITUO | KM | MADARAJA YA NAULI | | |
|---|---|---|---|---|
| | | DARAJA LA TATU | DARAJA LA PILI KUKAA | DARAJA LA PILI KULALA |
| KAHE | 20 | 4500 | 6400 | 10600 |
| KISANGIRO | 40 | 4,900 | 7,000 | 11,700 |
| SAME | 99 | 6,300 | 8,900 | 14,800 |
| MAKANYA | 133 | 7,100 | 10,200 | 16,900 |
| HEDARU | 152 | 7,600 | 10,800 | 18,000 |
| MKOMAZI | 184 | 8,500 | 12,100 | 20,100 |
| MOMBO | 223 | 9,400 | 13,400 | 22,200 |
| KOROGWE | 267 | 10,300 | 14,600 | 24,300 |
| MNYUZI | 282 | 10,700 | 15,300 | 25,400 |
| GENDAGENDA | 328 | 11,600 | 16,500 | 27,500 |
| MKALAMO | 355 | 12,000 | 17,200 | 28,600 |
| WAMI | 407 | 13,400 | 19,100 | 31,700 |
| DAR ES SALAAM | 558 | 16,500 | 23,500 | 39,100 |



### MAMBO YA KUZINGATIA UNAPOTAKA KUSAFIRI NA TRENI

A. Fika na kimoja kati ya vifuatavyo utakapotaka kukata tiketi
1. Kitambulisho cha Kura
2. Kitambulisho cha Taifa
3. Leseni ya Udereva
4. Kadi ya Bima ya Afya
5. Hati ya Kusafiria (Passport)
6. Barua ya Serikali ya Mtaa yenye picha ya Msafiri
7. Cheti cha Kuzaliwa kwa watoto au Barua ya Serikali za Mitaa

B. Uzito wa Mizigo
Treni ya Deluxe
1. Daraja la Pili Kulala Kilogramu 40
2. Daraja la Pili Kukaa Kilogramu 30
3. Daraja la Tatu Kilogramu 20

Treni ya Ordinary
1. Daraja la Kwanza Kilogramu 70
2. Daraja la Pili Kilogramu 40
3. Daraja la Tatu Kilogramu 20

Endapo uzito utazidi abiria atalazimika kulipia kiasi cha mzigo kilichozidi.

**Chukua Tahadhari unapokuwa karibu na Miundombinu ya reli ni Hatarishi**

# Treni ya Kisasa ya Deluxe




Muonekano wa nje ya Treni ya kisasa Deluxe.
Treni hii ina behewa za abiria daraja la tatu kukaa, la pili kulala na la pili kukaa pamoja na behewa maalum kw aajili ya chakula na vinywaji kemkem





Daraja la Pili Kulala



Daraja Pili Kukaa



Daraja la Tatu Kukaa

## RATIBA YA TRENI YA ABIRIA YA DELUXE
## DAR ES SALAAM - MOSHI - DAR ES SALAAM

| SIKU | KITUO | MUDA WA KUONDOKA | KITUO | MUDA WA KUWASILI |
|---|---|---|---|---|
| **KUTOKA DAR ES SALAAM KUELEKEA MOSHI** | | | | |
| JUMATATU | KAMATA | SAA 10:30 ALASIRI | MOSHI | SAA 02:30 ASUBUHI |
| JUMATANO | KAMATA | SAA 10:30 ALASIRI | MOSHI | SAA 02:30 ASUBUHI |
| IJUMAA | KAMATA | SAA 10:30 ALASIRI | MOSHI | SAA 02:30 ASUBUHI |
| **KUTOKA MOSHI KUELEKEA DAR ES SALAAM** | | | | |
| JUMANNE | MOSHI | SAA 10:30 ALASIRI | KAMATA | SAA 02:30 ASUBUHI |
| ALHAMISI | MOSHI | SAA 10:30 ALASIRI | KAMATA | SAA 02:30 ASUBUHI |
| JUMAMOSI | MOSHI | SAA 10:30 ALASIRI | KAMATA | SAA 02:30 ASUBUHI |

### TAHADHARI

Watumiaji wa Barabara katika mikoa ya Pwani, Tanga, Kilimanjaro (na baadae Arusha) Wanatakiwa kuhakikisha wanasimama mita 2.5 kutoka katika makutano ya reli na barabara ili kuhakikisha usalama wao, vyombo vyao na wanyama kabla ya kukatiza ili kuepusha ajali

### VITUO VYA KUKATA TIKETI

KAMATA DAR ES SALAAM
RUVU |WAMI | MKALAMO
GENDAGENDA | MNYUSI |
MOMBO | MKOMAZI | HEDARU
MAKANYA SAME | KISANGIRO
KAHE | MOSHI | KOROGWE

### KUMBUKA;

Nauli ya Mtoto Chini ya Miaka 6 ni Bure, Kuanzia miaka 7 hadi miaka 13: Atalipa nusu ya nauli ya Mtu mzima kwa madaraja yote na atapata siti yake

Ulinzi wa Miundombinu yareli ni jukumu letu sote. hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote atakayehujumu

Inashauriwa kufuata taratibu na maelekezo kutoka kwa wahudumu wa treni ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza unaposafiri na treni







Mtandao wa Reli wa TRC

## RAIS WA JAMHURI YA KIDEMOKRASIA YA KONGO AMPONGEZA JPM KWA UJENZI WA RELI YA KISASA - SGR.



Wairi wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhandisi Isack Kamwelwe akimuelezea Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo Mhe. Felix Tshisekedi kuhusu maendeleo ya Mradi wa SGR eneo la Vingunguti Dar es Salaam Desemba 2019.

Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo Mhe. Felix Tshisekedi Tshilombo atembelea mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR kipande cha Dar es Salaam - Morogoro, ziara hiyo imefanyika June 2019.

Ziara hiyo iliongozwa na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadosa na viongozi wa ngazi ya Kitaifa, ambapo Rais alipata fursa ya kuona hatua tofauti za ujenzi wa reli ya kisasa ukiwemo utandikaji wa reli ya kisasa - SGR unaoendelea maeneo ya Vingunguti jijini Dar Es Salaam.

Aidha, Rais Felix Tshisekedi amesema kuwa lengo la ziara nchini Tanzania ni kuthibitisha mahusiano kati ya nchi ya Kongo na Tanzania kupitia ujenzi wa miundombinu ambayo itasaidia kujenga uhusiano wa sekta ya biashara, uchumi na viwanda kati ya Kongo na Tanzania.

Hata hivyo, Rais Felix Tshisekedi alitoa pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa uthubutu na juhudi anazofanya hasa kwenye kuimarisha miundombinu ukiwemo ujenzi wa reli ya kisasa ambao ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi wa Tanzania na nchi jirani.

Mh.Rais wa Kongo ameishauri Tanzania kutunza na kudumisha miundombinu ili kuongeza uchumi wa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Naye, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhandisi Kamwelwe alibainisha kwa kueleza jinsi sekta ya usafirishaji wa njia ya reli nchini Tanzania utakavyo shirikiana na nchi ya Kongo pamoja na nchi za maziwa makuu katika usafirishaji wa mizigo ambao utakuwa ni tija katika ukuaji wa uchumi barani Afrika.



*Rais wa Jamhuri ya Demokrasia ya Congo Mhe Felix Antoine Tshisekedi Tshilombo akitembea kwenye kipande cha Reli ya kisasa - SGR kilichotandikwa katika eneo la vingunguti Dar-es-salaam Juni 2019.*

## WAZIRI WA UWEKEZAJI NA VIWANDA SUDAN ATEMBELEA MRADI WA UJENZI YA RELI YA KISASA - SGR

Waziri wa Viwanda na Uwekezaji Sudan Kusini Ndugu Paul Mayomu atembelea Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa-SGR kipande cha Dar es Salaam - Morogoro, ziara hiyo imefanyika Juni, 2019.

Aidha, katika ziara hiyo iliongozwa na mwenyeji wake Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhandisi Isaac Kamwelwe, walipata fursa ya kuona maendeleo na hatua tofauti za ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR ukiwemo ujenzi wa stesheni kuu ya Daresalaam, madaraja, na utandikaji wa reli unao endelea maeneo ya vingunguti jijini Dar Es Salaam.

Waziri Mayomu ameipongeza Tanzania kwa ujenzi wa SGR ambayo ni muhimu katika kuchochea maendeleo ya uchumi, viwanda na biashara katika taifa na nchi jirani.

Hata hivyo, Waziri Mayomu ameeleza kuwa reli hii itakapokamilika itakuwa chachu ya maendeleo kwa nchi zote mbili pia itadumisha uhusiano katika sekta ya uchukuzi, viwanda na biashara kati ya Tanzania na Sudan ya Kusini.

Aidha, Waziri Kamwelwe amempongeza waziri Mayomu kwa kuja Tanzania kwa kutembelea na kujionea maendeleo yanayofanyika katika sekta ya usafirishaji na uchukuzi.



*Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasliano Mhe. Mhandisi Isack Kamwelwe akimuonesha Waziri wa Viwanda na uwekezaji Sudan Kusini Mhe. Paul Mayon kubora wa Mataruma na Reli ya kisasa katika eneo la vingunguti Dar es Salaam Juni 2019.*

## VIONGOZI WA JUMUIYA YA WAZAZI CCM WATEMBELEA MRADI WA SGR

Na Mwandishi wetu TRC



Viongozi wa Jumuiya ya Wazazi CCM wakipata ufafanuzi kutoka kwa Meneja Msaidizi Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa Dar es Salaam - Morogoro Mhandisi Ayoub Mdachi kuhusu Ujenzi wa Daraja la treni lenye urefu wa KM 2.5 Ilala Dar es Salaam, Novemba 2019.

Viongozi wa Jumuiya ya Wazazi Chama cha Mapinduzi Taifa wakiongozwa na Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo Dkt. Edmund Mndolwa wametembelea Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR kipande cha Dar es Salaam – Morogoro eneo la Vingunguti hadi Stesheni jijini Dar es Salaam Novemba, 2019.

Viongozi hao wamefanya ziara hiyo kwa lengo la kuona maendeleo ya mradi, kujifunza pamoja na kukagua utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015/20 inayotekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli.

Katika ziara hiyo viongozi walipata fursa ya kuona kazi tofauti za Mradi wa SGR ambao kwa majumuisho zimefikia zaidi ya 72% kwa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro, sambamba na hayo walipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa kuhusu mabadiliko yanayoendelea kufanyika katika shirika ili kukidhi haja ya watanzania ya kupata usafiri wa uhakika na kufikia Tanzania ya viwanda na uchumi wa kati.

Wakiwa katika eneo la Vingunguti viongozi wa Jumuiya ya Wazazi CCM walipata maelezo kuhusu Mradi kutoka kwa Mhandisi Ayubu Mdachi ambaye ni Meneja Mradi Msaidizi kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro ambaye amesema kuwa mradi umefika zaidi ya 72% huku zoezi la uwekaji wa miundombinu ya umeme ukiwa umefika 62%.

Akizungumza kwa niaba ya wenyeviti wa Mikoa, Mwenyekiti wa Jumuiya wa wazazi Mkoa wa Mwanza Ndugu Nyiliza Makongoro amesema kuwa wameridhishwa na kasi ya ujenzi wa mradi huo wa reli ambao unasimamiwa na wazawa kwa asilimia kubwa.

Aidha Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa aliwashukuru viongozi hao kwa kuutembelea Mradi wa SGR na kuwaambia kuwa TRC inatarajia kufungua njia ya Tanga hivi karibuni na safari inatarajiwa kuanza Desemba 6, 2019.

"Kwa niaba ya Serikali tunafungua reli ya kaskazini Dar es Salaam - Kilimanjaro kwa kuanza majaribio Tarehe 01 Desemba 2019, na tutaanza safari rasmi Tarehe 06 Desemba 2019, dhamira yetu ni kufika Arusha ambapo ukarabati wake mpaka sasa umefika zaidi ya 85%".

## UVCCM CHAMWINO WATEMBELEA MRADI WA RELI YA KISASA

Shirika la Reli Tanzania limepokea ugeni kutoka Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Kutoka Wilaya ya Chamwino Mkoani Dodoma hivi karibuni kwa lengo la kupata fursa ya kutembelea na kuona maendeleo ya mradi unaoendelea wa ujenzi wa reli ya kisasa kuanzia Dar es Salaam hadi Kilosa mkoani Morogoro.

Akizungumzia ziara hiyo Meneja Mradi Msaidizi kutoka Dar es Salaam - Morogoro Mhandisi Ayoub Mdachi amesema kuwa ujio huu wa UVCCM ni muhimu kwani vijana wanapata nafasi ya kujionea wenyewe kinachoendelea kufanyika katika mradi ili kwenda kuwakilisha vyema kwa wananchi juu ya Serikali ya awamu ya tano inavyoleta maendeleo kwa kasi zaidi na kuhakikisha kazi zinafanyika mchana na usiku.

Vijana hao walipata fursa ya ufafanuzi juu ya mradi mzima wa SGR kutoka kwa wahandisi wa mradi kwa kipande walichotembelea na kujifunza mambo mengi yanayohusiana na maswala ya kiufundi pamoja na kiuhandisi.

Naye Meneja Mradi Msaidizi kutoka Morogoro - Makutupora Mhandisi Christopher Mang'wela ameeleza kua vijana wengi walioko nje ya mradi hawana uelewa wa kinachoendelea kuhusu ujenzi wa SGR hivyo kupitia UVCCM Chamwino wataiwakilisha vyema Serikali juu ya mradi huu unaoenda kwa kasi.

Katibu wa Umoja wa Vijana CCM wilaya ya Chamwino Peter Dafi amesema kuwa wamefurahishwa sana na ziara hii kwani wamejifunza na kujionea ujenzi wa mradi wa SGR unavyoendelea kwa kasi ambayo Shirika la Reli pamoja na Serikali ya awamu ya tano imekua ikiwekeza nguvu na juhudi ili kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati.

## RAIS WA BENKI YA MAENDELEO YA BIASHARA KUSINI NA MASHARIKI MWA AFRIKA AFURAHISHWA NA MRADI WA SGR

Na Mwandishi wetu TRC



*Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa (kati) na Rais wa Benki ya Maendeleo ya Biashara Dkt. Admass Tadesse (wa tatu kushoto) wakiwa katika picha ya pamoja na baadhi wa Viongozi kutoka TRC, Yapi Merkezi, KORAIL na Maafisa walioambatana na Dkt. Admass Tadesse.*

Rais na Mtendaji Mkuu wa Benki ya-Maendeleo ya Biashara Mashariki na Kusini mwa Afrika (TDB) Dkt. Admassu Tadesse ameipongeza Serikali ya Tanzania kwa kutekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa - SGR kwa kutumia fedha zake za ndani na kuahidi kuwa Benki yake itafanya kila linalowezekana kuhakikisha inatafuta fedha za kujenga reli hiyo.

Dkt. Tadesse ametoa kauli hiyo alipotembelea sehemu ya ujenzi wa miundombinu ya reli hiyo, kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro na kujionea kazi kubwa iliyofanyika ambapo amesema mradi huo hautainufaisha Tanzania pekee bali pia nchi za ukanda wa Afrika hususani ambazo hazipakani na bahari.

Aliahidi kuwa kwa kuwa fedha zinazohitajika kukamilisha ujenzi wa mradi huo wa reli ya kisasa ni nyingi, Benki yake itazishawishi taasisi nyingine za fedha ndani na nje ya Bara la Afrika kuchangia ujenzi huo ili mradi ukamilike kwa wakati na kuchochea uwekezaji, Biashara na kuboresha shughuli za usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndg. Masanja Kadogosa, ameishukuru Benki hiyo kwa kuonesha nia ya kusaidia ujenzi wa Reli hiyo katika awamu zijazo

Alisema kuwa mpaka sasa ujenzi wa Reli ya Kisasa ambao umetumia fedha za ndani kati ya Dar es Salaam hadi Morogoro umekamilika kwa asilimia 72 huku kipande cha Morogoro hadi Makutupora mkoani Singida kikiwa kimekamilika kwa asilimia 22.

Bw. Kadogosa amesema kuwa Serikali inatafuta fedha nyingine kwa ajili ya kujenga reli hiyo kuanzia Makutupora, Tabora, Isaka hadi Mwanza na kwamba watafanya mazungumzo na Benki hiyo kuona namna watakavyofadhili ujenzi huo.

## MAWAZIRI WA MAMBO YA NJE WA NCHI ZA NORDIC NA AFRIKA WATEMBELEA MRADI WA SGR

Na Mwandishi wetu TRC

Mawaziri wa Mambo ya nje wa nchi za Nordic na Afrika watembelea Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro, kuanzia eneo la Stesheni hadi Vingunguti Dar es Salaam Novemba, 2019.

Lengo la ziara hiyo ni kuona hatua kubwa ambayo serikali ya Tanzania imepiga katika kuboresha miundombinu ya usafirishaji ukizingatia miundombinu ni moja kati ya vitu vinavyoimarisha uhusiano na ushirikiano baina ya nchi za Nordic na Afrika.

Mawaziri hao walipata fursa ya kuona maendeleo ya ujenzi wa stesheni ya reli ya kisasa inayojengwa eneo la stesheni jijini Dar es Salaam, daraja la treni lenye urefu wa KM 2.5 pamoja na maendeleo ya Mradi kwa ujumla kipande cha Dar es Salaam – Morogoro ambao umefikia zaidi ya 70%.

Miongoni mwa Mawaziri waliopata fursa ya kutembelea mradi ni kutoka nchini Egypt, Nigeria, Angola pamoja na Niger. Ziara hii ni matunda ya mkutano wa Mawaziri hao uliojadili mambo kadhaa kuhusu uhusiano na ushirikiano uliopo kati ya nchi za Afrika na nchi za Nordic uliofanyika katika ukumbi wa kimataifa wa mikutano wa Mwl. J.K Nyerere Dar es salaam.

Naye Waziri wa Mambo ya Nje nchini Nigeria Mhe. Zubairu Dada amesema kuwa amefurahishwa na emeipongeza Tanzania kwa kutumia fedha zake za ndani kujenga reli ya kiwango cha kimataifa kuanzia Dar es Salaam hadi Makutupora Singida.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa amewashukuru Mawaziri hao kwa kuamua kutembelea mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa.

# TRENI YA DELUXE ILIYOBEBA WASANII WA WCB YAWASILI KIGOMA NA KUPOKELEWA NA MAMIA YA WANANCHI

Na Mwandishi wetu TRC



*Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa akizungumzia safari ya wasanii wa WCB kwa kutumia treni ya kisasa ya Deluxe mara baada ya kuwasili katika Stesheni ya Kigoma ikitokea Dar es Salaam hivi karibuni Desemba 2019.*

Treni ya Kisasa ya Deluxe ya Shirika la Reli Tanzania - TRC iliyobeba wasanii wa muziki wa kizazi kipya kutoka kampuni ya Wasafi Classic Baby (WCB) imewasili mkoani Kigoma ikitokea Dar es Salaam hivi karibuni Desemba 2019.

TRC kwa kushirikiana na kampuni ya WCB hivi karibuni waliandaa safari kuelekea Kigoma kwa kutumia treni ya kisasa ya Deluxe kwa lengo la kuhamasisha watanzania kutumia usafiri wa treni, kutangaza huduma ya Miradi ya Shirika pamoja na kuhamasisha watanzania kulinda miundombinu ya reli.

Katika safari hiyo iliyohusisha wasanii zaidi ya 200 wa muziki wa kizazi kipya kutoka kampuni ya WCB na wasanii wengine wa muziki wa kizazi kipya ilikuwa pia na lengo la kuadhimisha miaka 10 ya Msanii ambaye pia ni Mkurugenzi wa Kampuni ya WCB Diamond Platnum katika tasnia ya muziki nchini.

Kama ambavyo abiria wengine wamekuwa wakipata fursa ya kufurahia safari ambayo huwa zaidi ya safari kwa kutumia treni, wasanii nao walipata fursa ya kuona mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR unaotekelezwa kuanzia Dar es Salaam hadi Makutupora Singida kwa fedha za watanzania wazalendo ambapo pia walitembelea

handaki namba mbili ambalo ni refu zaidi nchini lenye urefu wa KM 1.031 kwa ajili ya kupitisha reli ya SGR Kilosa mkoani Morogoro.

Aidha wasanii hao wameonekana kufurahishwa na huduma za treni ya kisasa ya Deluxe tangu mwanzo hadi mwisho wa safari kutokana na huduma nzuri pamoja na burudani zinazopatikana ndani ya treni

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kadogosa amesema kuwa wasanii hao wameonesha uzalenda wa aina yake kwa kujali vya kwetu, kwani wametoa muda wao na fedha zao kutumia usafiri wa treni kwa lengo la kuutangaza usafiri huu pamoja na Shirika kwa ujumla, kwa kipekee ametoa shukurani kwa wasanii wa WCB kwa uzalendo wao.

Nasib Abdul maarufu kama Diamond Platnum kwa niaba ya Kampuni ya WCB amemshukuru Mkurugenzi Mkuu wa TRC kwa utayari aliouonesha tangu siku ambayo walipeleka maombi ya safari hiyo na ushirikiano uliokuwepo katika safari kuanzia Dar es Salaam hadi Kigoma.



*Msanii wa Muziki wa kizazi kipya Diamond akiwa na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli alipomtembelea kwa ajili ya mazungumzo ofisini kwake Makao makuu TRC jijini Dar es Salaam.*





*Picha zikionesha matukio tofauti safarini kabla ya treni ya Deluxe kuwasili Kigoma*





*Picha zikionesha matukio tofauti mara baada ya treni ya Deluxe kuwasili Kigoma*

**Katika kuadhimisha Wiki ya TRC baadhi ya wateja walipata fursa ya kutoa maoni ambapo Maafisa kutoka Shirika la Reli Tanzania – TRC waliwatembelea baadhi ya wadau wanaotumia usafiri wa reli kwa kusafirisha mizigo mbalimbali kutoka sehemu moja kwenda nyingine, wadau hao ni kampuni ya Bakhresa na Kampuni ya YARA.**
**Haya ni baadhi ya maswali na majibu kwa wadao hawa**

**SWALI: Una maoni gani?**
**JIBU:** Maboresho ni makubwa na yana muelekeo chanya kwa upande wa huduma za Shirika la Reli Tanzania nalishauri shirika kuimarisha mawasiliano pamoja na kuongeza mabehewa kwa ajili ya kutoa huduma kwa wakati na kuweza kupeleka mzigo mwingi kwa wakati.
**SWALI: Unazionaje Huduma za TRC?**
**JIBU:** Wadau tunatarajia huduma nzuri kwa kuwa zimeboreshwa zaidi lakini kuna umuhimu kubwa sana wa kuongeza mabehewa na mawasiliano ya karibu zaidi kuhusu taarifa za uwepo wa mabehewa matupu, na mabehewa mangapi yako tayari kwa kubeba mzigo. Sisi tuna nanategemea muongozo kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania – TRA kwamba kuna muda tunatakiwa kukamilisha kutoa mzigo.
Tumekuwa tukishirikiana kwa ukaribu sana na Shirika la reli na mpaka sasa huduma tunazopata zina muelekeo chanya kablsa na kwa maboresho haya tuna matumaini makubwa kwamba tutaweza kusafirisha mizigo yetu kwa idadi kubwa zaidi
**SWALI: Unazungumziaje mageuzi yanayoendelea katika Shirika**
**JIBU:** Mageuzi yanayoendelea katika sekta ya reli nchini yanaweza kuleta tija kubwa kwa Shirika na Wateja wake, kwa sababu kuna *'economic of scale'* upande wa movement ya mabehewa katika kila behewa tatu ni sawa na roli nne za tani 30 unakuwa umeokoa roli moja hivyo itapunguza gharama za usafirishaji vilevile itasaidia kuokoa barabara zetu kuharibika lakini pia zipo bidhaa nyinyi ambazo zinatakiwa bandarini kwa hiyo ni vizuri kuwa na mawasiliano ya karibu na kujua idadi kamili ya mabehewa matupu ambayo yanakidhi kubeba mzigo bandarini. kusafirishwa kwa reli na si maroli, kwahiyo basi shirika linatakiwa kuboresha vichwa vya treni na mabehewa ili kusaidia kubeba mizigo mingi.
**SWALI: Je, mnaridhika na huduma za TRC?**
**JIBU:** Huduma mpaka sasa ni bora na zinaridhisha lakini zinaweza kuwa bora zaidi kama shirikalitaweza kusafirisha bidhaa zetu kwa wingi katika maeneo mbalimbali.
Mpaka sasa jitihada zinazofanywa na Serikali katika sekta ya reli zina matokeo chanya kwahiyo serikali iendelee kukamilisha jitihada hizo ili shirika liweze kutoa huduma bora kwa wateja.




*Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Kampuni ya BAKHRESA Dkt. Ally Sabuni akifanyiwa mahojiano na Bi. Tracylinda Nganga, Afisa habari wa TRC katika ofisi Ya BAKHRESA jijini Dar es Salaam*

# Mageuzi yanayoendelea katika usafiri wa reli ni muhimu, YARA wathibitisha

**SWALI: Una maoni gani kuhusu hudua za TRC?**

**MAJIBU:** Kwa upande wa huduma TRC wanatakiwa kuongeza ufanisi katika utoaji taarifa kwa maana ya kwamba ni wakati gani mteja anaweza kupata behewa na kupata taarifa za behewa wakati zikiwa njiani kwa maana ya kwamba tunahitaji kupata taarifa za maendeleo ya mzigo punde unapotoka Dar es Salaam kuelekea Mikoani hilo linaweza kutusaidia sisi kama wateja kuwasiliana na watu wanaopokea mzigo unakoelekea ili kuongeza ufanisi katika ushushaji wa mizigo, lakini pia itatusaidia kujua behewa zetu zimesha pakia, zimeshaondoka na zimefika sehemu fulani hiyo itamrahisishia mteja kujiandaa kwa kupokea mzigo lakini pia kuokoa muda.

**SWALI: Unazungumziaje mapinduzi yanayofanyika katika sekta ya reli nchini?**

**MAJIBU:** Mageuzi yanayoendelea katika sekta ya usafirishaji na uchukuzi hasa upande wa usafiri wa reli ni kitu cha muhimu sana na ndicho



kitu pekee kinachoweza kuisaidia TRC kufanya kazi vizuri zaidi na pia sisi kama wateja kunufaika na huduma ambazo tunapata lakini pia wakulima ambao pia ndio walengwa wakuu katika hii huduma na wao kupata mbolea kwa wakati na kwa bei nafuu zaidi kwa sababu ukilinganisha gharama za kusafirisha mbolea kwa njia ya reli na magari nafikiri ni nusu ya gharama zinaweza kupungua kama tutatumia njia ya reli, hiyo gharama inayopungua ndiyo itakayomsaidia mkulima kupungua kwa gharama ya mbolea. Sisi kama YARA tukiangalia mpaka sasa tumefanikiwa kuwapunguzia wakulima kiasi fulani cha gharama kwa sababu tunatumia njia ya reli kwahiyo tunatumia gharama kidogo za usafirishaji hivyo inatupunguzia gharama ya mwisho ya kuuzia mbolea. Kwahiyo ni vizuri mageuzi hayo yasichukue nguvu ili tuweze kuendana na kasi ya Mheshimiwa Rais.

**SWALI: Je, huduma zinazotolewa na TRC zinakidhi mahitaji yenu?**

**MAJIBU:** Sisi kama Kampuni ya YARA tumeridhika na huduma inayotolewa na Shirika la Reli Nchini kwa namna inavyofanya kazi na tukiangalia historia ilivyokuwa hapo nyuma, tunaomba wazidi kuongeza nguvu ili huduma iwe bora zaidi.

Juhudi zinazoendelea katika uboreshaji wa mabehewa ziende sambamba na uboreshaji wa njia za reli kwa maana ya kwamba vitu vyote hivl vinategemeana na vikiboreshwa vyote huduma zitakuwa bora zaidi.

# TRC; Watanzania watarajie huduma bora katika treni za reli ya kisasa - SGR



*Henry Machoke, Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Biashara TRC.*

**SWALI: WANANCHI WATARAJIE NINI KATIKA SUALA ZIMA LA USAFIRISHAJI KWA MWAKA 2020/21**

**JIBU:** Watanzania watarajie kupokea reli mpya ya SGR na kupanda treni mpya ambazo zitatembea kwa mwendokasi Kilomita 160 kwa saa na treni hizo zitakuwa ni za kisasa na mpya tofauti na hii tuliyonayo kwa sasa, lakini si hivyo tu reli ya SGR kwa upande wa huduma zitakuwa bora zaidi ndani ya treni kutakuwa na wahudumu tofauti, huduma za kisasa kama 'internet' kwa njia nzima mpaka Morogoro, lakini pia kutakuwa na burudani mbalimbali wateja wataangalia Sinema wakiwa ndani ya treni hivyo safari itakuwa fupi na ya starehe zaidi.

Kwa upande wa treni ya mzigo treni hii itapunguza muda wa kusafirisha mzigo kwa mfano treni ya mzigo kwa ikitoka Dar es Salaam mpaka Kigoma nakurudi inatumia zaidi ya siku 21 hivyo reli hii ya kisasa itasaidia sana katika swala zima la kuokoa muda na kufanya treni kusafirisha mizigo mara nyingi kwa wakati.

**SWALI: KUNA HUDUMA YOYOTE MPYA AMBAYO INATARAJIA KUANZISHA ILI KUONGEZA PATO LA SHIRIKA?**

**JIBU:** Tunategemea Reli ya Kisasa - SGR itakapoanza kufanya kazi zipo njia nyingi zitakazo tumika kuingiza pato kwa shirika moja wapo ni treni yenyewe ambayo itaingiza pato kwa shirika kwa njia ya usafirishaji abiria na mizigo lakini pia kupitia stesheni zetu tutaingiza pato pia kwani stesheni zetu hasa hii kubwa ya Dar es Salaam itakuwa na vituo vya biashara kama Benki, Hotel, Maduka, sehemu za burudani, maegesho ya magali, sehemu zote hizo zitakuwa zinaingiza pato kwa Shirika lakini pia kwa siku za usoni tutaweka utaratibu kwa wale wote wanaowasindikiza wasafiri wakitaka kuingia watalipia kiasi kidogo ambacho nacho kitachangia kukuza pato la Shirika na taifa Kwa ujumla.

**SWALI: HALI YA BIASHARA IKOJE SHIRIKA KATIKA?**

**JIBU:** Kwa suala la usambazaji na uhitaji kwa sasa ni changamoto kwani Uhitaji ni mkubwa kuliko usambazaji kwenye treni yetu ya abiria kwahiyo mpaka hapo tunaona uhitaji wa mabehewa ni mkubwa, aidha mbali na changamoto hali ya biashara imezidi kuimarika katika Shirika.

Tunaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwani tunatarajia kupokea mabehewa 45 ya abiria ifikapo mwaka 2020, lakini pia Serikali inaendelea na mradi wa ukarabati wa mabehewa 200 ikiwa ni sehemu ya mkakati wa serikali kukarabati mabehewa 700 - 1000 ya mizigo.

**SWALI: MIPANGO YA TRC KATIKA USAFIRISHAJI WA MIZIGO HASA MAZAO YA KILIMO DAR - MOSHI?**

**JIBU:** Reli ina mchango mkubwa sana katika kukuza uchumi wa nchi, inasaidia kusafirisha malighafi kutoka eneo la uzalishaji kwenda sokoni. Kwa ujio wa safari mpya ya Dar es Salaam mpaka Moshi kwa upande wa treni za mizigo imekuwa na mchango mkubwa kwa wakulima wa mikoa ya kaskazini ambao ni wakulima wa ndizi, mbogamboga na mazao mengine mengi hata kwa upande wa wafanyabiashara wa vitoweo kama Samaki wameonesha nia ya kutumia usafiri wetu wa reli kwa kubainisha changamoto wanazopata katika kusafirisha kwa kutumia gari na kusababisha vitoweo kuharibika na kutofika sokoni kwa wakati. Mwisho kabisa treni hii itaongeza ajira kwa wanakaskazini kwa kutumia fursa hii kujiajiri katika sekta ya Kilimo kutokana na uhakika wa usafiri.

Na Mwandishi wetu TRC



**SALIM ABDALLAH**
MKAZI WA DAR ES SALAAM

"Nampongeza Rais Magufuli kwa utekelezaji huu alioufanya wa mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa, na kupitia kauli yake ya HAPAKAZITU vijana wetu wamepata ajira kupitia ujenzi huu na tunaona wanaendelea na ujenzi usiku na mchana hili ni jambo zuri linapunguza vijana kutokaa bila kazi majumbani na badala yake wanafanya kazi ambayo Mheshimiwa Rais anaitaka kwa maslahi ya nchi yetu"



**ASSAY NICODEMUS**
MKAZI WA MPWAPWA
MKOANI DODOMA

"Jambo ambalo sikulitegemea ni serikali kutulipa wananchi fidia ya maeneo yetu kwa wakati, ila naishukuru Serikali yangu kwa kuwa na uharaka wa kutupatia fidia na kufanya ujenzi huu uende kwa kasi ili wananchi tuanze kutumia treni ya mwendokasi tuondokane na tabu tunayoipata ya usafiri na kutumia masaa mengi barabarani"



**ALLY MOHAMMED**
MKAZI WA DAR ES SALAAM

"Wananchi tuna hamu kubwa ya kuona hii treni ya mwendokasi ikianza misafara, tukiona huu ujenzi wa mradi wa SGR unaendelea unatupa hamasa, tunaamini ukikamilika utabadilisha maisha ya Watanzania wengi"



**JOSEPH SEBASTIAN**
MKAZI WA DAR ES SALAAM

"Mradi huu wa ujenzi wa reli ya kisasa umetufumbua macho watanzania wengi na kuona kwamba serikali ikiamua inaweza kuleta mabadiliko kwa wananchi wake hasa wa hali ya chini na tunategemea kusafiri kwa gharama nafuu kulingana na hali halisi ya wananchi"



**SHABANI SELEMANI**
AFISA MTENDAJI
KIJIJI CHA GODEGODE
WILAYA YA MPWAPWA

"Mradi huu wa ujenzi wa reli ya kisasa umetuletea mafanikio makubwa katika kijiji chetu hapa Godede kwani vijana wengi wamepata ajira kupitia mradi, changamoto ya barabara imepungua kwani muda mwingine tunatumia njia za mradi, vilevile wananchi wamefurahia kuachia maeneo ili kupisha maendeleo na kupata malipo yao kwa wakati"

# MIAKA 4 YA MAFANIKIO YA UONGOZI WA SERIKALI YA AWAMU YA TANO KATIKA SEKTA YA RELI NCHINI

Na Mwandishi wetu TRC

Katika kuboresha uendeshaji wenye tija kwa maslahi ya Tanzania, Serikali ilifanya maamuzi ya kuunganisha taasisi mbili za reli yaani Kampuni ya Reli Tanzania - TRL na Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli - RAHCO na kuanzisha Shirika la Reli Tanzania - TRC ambalo lilianza kai rasmi mwezi Machi 2018.

Katika kipindi cha miaka minne jumla ya Tani 1,456,537 za mizigo zimesafirishwa katika reli ya kati (Dar. Mwanza na Kigoma), Tani 52,709 za mizigo zimesafirishwa tangu kufunguliwa kwa usafiri wa reli kati ya Dar es Salaam na Kampala na Tani 3,860 za mizigo zimesafirishwa tangu kufunguliwa kwa reli ya Tanga – Moshi. Hata hivyo abiria wa treni za mikoani wameongezeka kutoka 411,172 mwaka 2014/15 hadi 578,439 mwaka 2018/19.

Mapato ya Shirika yameongezeka kutoka SHS. 17,410,602,717 mwaka 2014/15 hadi SHS. 30,041,773,815 mwaka 2018/19 kwa treni za mizigo, kutoka SHS. 8,390,387,802 hadi SHS. 10,774,121,092 kwa treni za abiria wa mikoani na SHS. 316,668,300 hadi SHS. 1,968,474,300 mwaka kwa treni za mjini sawa na abiria 845,607 kwa mwaka 2014/15 hadi abiria 4,280,043 mwaka 2018/19.

Halikadhalika Serikali kupitia TRC imeazimia kujenga reli ya kisasa - SGR yenye mtandao usiopungua KM 2,561 kuunganisha mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma, Katavi na nchi zisizokuwa na bandari (Rwanda, Burundi, DRC). Kazi za mradi zinaendelea katika kipande cha kwanza cha Dar es Salaam - Morogoro, ambacho kimefikia asilimia zaidi ya 70% na kipande cha Morogoro - Makutupora Singida ambacho kimefikia zaidi ya asilimia 20%. Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Tanzania kwa kutumia fedha za ndani kwa 100%.

Mradi huu utakapokamilika Shirika litaweza kusafirisha mizigo mingi zaidi, treni moja ya mizigo itaweza kubeba Tani 10,000 kwa mkupuo, hivyo itawezesha kuchochea maendeleo ya shughuli nyingi za kiuchumi (viwanda, kilimo, na biashara), kiutawala na kijamii. Aidha zaidi ya watanzania 14,000 wamepata ajira za moja kwa moja pia wakazi wa maeneo ya mradi wamepata fursa ya kufanya biashara wakiwemo mama ntilie.

Sambamba na mradi wa SGR Serikali ya awamu ya tano kupitia TRC inatekeleza mradi wa Uboreshaji wa reli ya Kati - TIRP Dar es Salaam - Isaka (KM 970) chini ya Mkandarasi 'China Civil Engineering and Construction Corporation' (CCECC), mradi unagharimu pesa za kimarekani Dola Milioni mia tatu ($ 300,000,000).. Lengo la mradi wa TIRP ni kuongeza ubora na uimara wa njia ya reli ya kati kutoka Dar es Salaam hadi Isaka ili iweze kubeba mizigo kutoka chini ya Tani 13.5 za uzito wa eskeli hadi Tani 18.5 na kutoka mwendokasi wa KM 35 hadi KM 70 kwa saa ili kuongeza ufanisi na uhakika wa huduma.

Mradi unahusisha utandikaji wa reli zenye uzani wa paundi 80 kwa urefu wa kilometa 312, ukarabati njia za reli kwa urefu wa Kilometa 658, makalavati na madaraja 442, uboreshaji mfumo wa mawasiliano, ukarabati wa vituo vya kupakia na kupakua mizigo vya bandari ya Dar es salaam, Ilala na Bandari kavu ya Isaka, ununuzi wa mitambo ya ukarabati wa njia, ukarabati wa vichwa viwili vya treni, ununuzi wa vichwa vitatu vya treni na mabehewa 44 ya mizigo.

Mradi wa TIRP umezalisha ajira zaidi ya 1600 na kukuza kipato cha watanzania ambapo, wafanyabiashara na watoa huduma mbalimbali wamenufaika. Pia umesaidia kuwajengea ujuzi watanzania wanaoshiriki katika shughuli za ujenzi, mpaka sasa wapo watanzania wanaosimamia na kufanya kazi za ujuzi katika mradi huu ikiwemo kuunga reli, kunyoosha na kushindilia reli. Halikadhalika mradi unatarajia kupunguza muda wa kupakia na kupakua mizigo kutoka Bandari ya Dar es salaam hadi Bandari kavu ya Isaka kufikia saa 24.

Majukumu ya Shirika la Reli Tanzania ni kutoa huduma za usafiri wa abiria pamoja na treni za Mizigo ndani na nje ya nchi, hivyo TRC imerejesha safari za treni za Mizigo kutoka Dar es Salaam hadi Kampala nchini Uganda kupitia Ziwa Victoria, takribani miaka 10 iliyopita safari hizi zilikuwa zimesitishwa na mnamo Julai 2019 Shirika limetimiza mwaka mmoja tangu kufunguliwa kwa huduma za usafiri wa treni Dar es Salaam - Kampala.

Aidha Shirika limefanikiwa kuboresha huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo kwa kuongeza vichwa vipya 11 vya njia kuu na kukarabati mabehewa 74 kati ya 200 chini ya ufadhili wa serikali na behewa 20 kati ya 40 kwa ufadhili wa Mpango wa Chakula Duniani - WFP pamoja na kuanzishwa kwa huduma ya usafiri wa mjini toka Dar es Salaam kwenda Pugu, huduma hii imerahisisha watu kuwahi sehemu za kazi na kurejea majumbani tofauti na ilivyokuwa awali.

Gharama za uendeshaji biashara kanda ya kaskazini zimepungua kufuatia kurejesha treni za mizigo kutoka Dar es Salaam - Tanga - Moshi huku mafundi wakiendelea kufufua njia ya reli kuelekea Arusha, hata hivyo huduma za treni za abiria zinatarajiwa kuanza mapema mwezi Desemba 2019.

## UKARABATI WA MABEHEWA KUWA CHACHU YA UKUAJI WA UCHUMI NCHINI KUPITIA USAFIRISHAJI WA MIZIGO

Na Mwandishi wetu TRC



*Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa wakikabidhiana na Muwakilishi wa Mpango wa chakula Duniani Bwana Michael Dunford makabrasha ya makubaliano ya ukarabati wa Mabehewa 40 ya mizigo katika karakana ya reli Dar es Salaam*

Tangu Rais wa awamu ya tano ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli aingie madarakani, ajenda kuu ya serikali ya Tanzania ni kuifanya Tanzania kuelekea uchumi wa kati na kuwa Tanzania ya viwanda ifikapo mwaka 2025.

Agenda hiyo imelenga kusisitiza mipango ya ukuaji na uboreshaji wa miundombinu wezeshi ikiwemo reli ili kuongeza ufanisi katika utendaji sambamba na kuhakikisha Tanzania inatimiza lengo la ukuaji wa uchumi na viwanda.

Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/19, Serikali imetenga jumla ya Shilingi bilioni 252.6 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya reli kupitia Mfuko wa Reli, haya yote yanafanyika ili kuimarisha miundombinu katika sekta ya usafirishaji wa reli nchini kwa maslahi ya taifa.

Maono ya Shirika la Reli Tanzania – TRC ni kutoa huduma bora, salama na ya kuaminika katika usafiri wa reli Afrika Mashariki na Kati, sanjari na maono hayo Shirika limejikita hasa kusimamia usafirishaji wa reli kwa gharama nafuu, utunzaji wa miundombinu ya reli na utoaji wa huduma za usafiri wa uhakika na salama kwa maendeleo endelevu ya uchumi wa Tanzania.

Ili kutimiza dhamira ya utendaji kazi kwa ufanisi, shirika linaendelea kuboresha miundombinu ya reli ili kuendeleza na kuhakikisha usafiri wa reli nchini unakuwa wa uhakika zaidi na kuchochea uchumi wa nchi kupitia sekta ya usafirishaji na uchukuzi katika kipindi hiki cha mchakato wa ujenzi wa viwanda nchini.

Jitihada zimeendelea kufanyika ambapo Serikali imekuwa ikiliwezesha Shirika kwa kutoa fedha kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya reli ili kuongeza ufanisi katika utendaji na sasa imeelekeza nguvu katika ukarabati wa mabehewa ambayo kwa muda mrefu yalikuwa yamechakaa na mengine kuharibika kutokana kukaa kwa muda mrefu bila kutumika.

Mapema, mwaka 2019 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli Kupitia Wizara ya Uchukuzi alitoa kiasi cha Shilingi Bilioni nne kwa TRC kwa ajili ya ukarabati wa mabehewa 200 ya mizigo kwa dhumuni la kuongeza ufanisi katika huduma ya usafirishaji mizigo nje na ndani ya nchi, kupunguza mrundikano wa mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam na kuongeza makusanyo ya Shirika.

kwa kawaida behewa hufanya kazi zaidi ya miaka 6 bila kufanyiwa matengenezo makubwa endapo halitapata ajali. Ukarabati wa behewa TRC uhusisha mfumo mzima wa behewa ukiwemo uboreshaji wa muonekano wa behewa (bodi) mfumo wa breki, baada ya kumaliza uboreshaji wa mfumo mzima behewa hupakwa rangi.

Kwa hivi sasa kazi ya ukarabati wa mabehewa inafanyika katika karakana kuu ya Reli jijini Dar es Salaam ambapo mafundi wa kila kitengo hufanya kazi zao kwa wakati, hivyo kupelekea kukarabati mabehewa matano (5) kwa wiki moja na kwa mwezi hukarabati mabehewa ishirini (20).

Gazeti la Reli na Matukio limezungumza na Mkurugenzi anayesimamia Mabehewa na Vichwa vya treni Mhandisi Albert Magandi ambaye amesema kuwa kazi kubwa inayoendelea ni ukarabati wa mabehewa yanayokidhi mahitaji ya wateja kulingana na aina ya shehena ya mzigo unaotakiwa kusafirishwa.

Mabehewa yanayofanyiwa ukarabati ni CCB (Container Carrier Bogie) - hubeba makontena, HLB(C) (High Large Bogie) - hubeba makontena, mabomba, mbao, magogo, na vyuma, CLB (Covered Large Bogie) - hubeba mizigo ya jumla kama vile Saruji, Sukari, Chumvi, Kahawa, Pamba, Tumbaku. BHB (Ballast Hopper Bogie) - hubeba kokoto, PTB (Petroleum Tank Bogie) - hubeba mafuta MGB (Motor Goods Bogie) - hubeba magari, CWB (Cattle Wagon Bogie) - hubeba mifugo. Aina hizi za mabehewa zitakapokamilika zitasaidia kusafirisha mizigo ndani ya Tanzania na nchi jirani za Burundi, Rwanda, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, kupitia bandari ya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma na Tanga.

Serikali ina jukumu la kusimamia maendeleo ya uchumi, kwa maana hiyo, moja ya madhumuni ya kiuchumi ni kutekeleza sera madhubuti ili kuhakikisha kuwa miundombinu sahihi ya usafirishaji inasaidia upatikanaji wa bidhaa na malighafi kwa bei nafuu na kukuza uchumi wa nchi. Kukamilika kwa Mradi huu awamu ya kwanza kutasaidia katika kukuza sekta za Maendeleo ikiwemo kilimo, viwanda, biashara, uwekezaji na mawasiliano nchini.

Serikali ina mpango endelevu wa kukarabati mabehewa 700 hadi 1000 ili shirika liweze kubeba mizigo inayoingia bandari ya Dar es Salaam na kusafirisha sehemu mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa ufanisi.

Hata hivyo kuna hitaji kubwa la Mabehewa ya kutosha kutokana na idadi na mizigo iliyopo Bandari ya Dar es Salaama na sehemu nyingine, pia uwepo wa miradi ya uboreshwaji wa miundombinu ya reli ni kiashiria tosha cha hitaji la Mabehewa na vichwa vya kutosha vitakavyofanya kazi katika reli inayoboreshwa kupitia mradi wa uboreshaji wa reli ya kati Tanzania - TIRP.

Uwekazaji unaondelea katika sekta ya Reli nchini inaonesha dhahiri Serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Jemedali, Rais Dkt. John Pombe Magufuli imedhamiria kuwa chachu katika ukuaji wa uchumi wa Tanzania na kutekeleza dhamira ya Tanzania kua ya Viwanda na uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.



*Mabehewa yakiwa yamekamilika kukarabatiwa katika karakana kuu ya reli jijini Dar es Salaam*

Na Dkt. Apolinary John

# AFYA NA HAKI ZA MFANYAKAZI BAADA YA KUUMIA KAZINI



Kumekuwa na uelewa mdogo kwa wafanyakazi pindi wanapopata ajali kazini wakiwa wanatekeleza majukumu yao kwa kushindwa kuelewa taratibu za kufuata ili kupata haki zao za msingi ambazo kwa mujibu wa sheria wanazostahili kupewa.

Leo ninapenda nieleze utaratibu mzuri ambao utamsaidia kila mtu kujipatia maarifa yatakayomsaidia yeye na wengine ambao yamkini hawajajua nini cha kufanya pindi wanapopata matatizo ya kiafya wakiwa kazini.

Tuanze kwa kujua makundi haya matatu, mosi kuna magonjwa ya kawaida, pili kuna magonjwa yanayotokana na kufanya kazi fulani na tatu ni ajali mbalimbali, aidha ajali zote ziwe za kawaida au za gari zina utaratibu.

Tukianza na magonjwa ya kawaida kama Malaria na Homa za matumbo, haya yakisharipotiwa katika kliniki zetu, wagonjwa huruhusiwa kwenda kutibiwa katika zahanati, vituo vya afya na hata hospitali za serikali za karibu.

Kwa kawaida magonjwa haya ya kawaida huwa hayana fidia. Kwa upande mwingine tukiangalia magonjwa yanayotokana na kazi au ajali zinazotokea wakati wa kufanya kazi ambazo zinahitaji fidia yana utaratibu ufuatao.

Kwa upande wa magonjwa, wataalamu wa afya watamchunguza, kisha kumweleza mgonjwa kwa kina ni jinsi gani kazi yake imepelekea yeye kupata madhara au ugonjwa na kumshauri endapo watabaini kuwa ugonjwa huo unatokana na kazi, pale ambapo watahitaji ushauri na matibabu ya kitaalamu zaidi madaktari humshauri mgonjwa na hata kuratibu rufaa yake.

Mgonjwa akishamaliza matibabu/ ufuatiliaji wa afya yake na tathmini ya uzito wa tatizo lake, watoa huduma za afya hujaza fomu maalumu kwenda katika mamlaka husika ya kutoa fidia kwa wafanya kazi (Workers Compensation Fund).

Fomu hizo hupelekwa kwa madaktari walioteuliwa kuthibitisha magonjwa hayo na namna matibabu yalivyofanyika na hatimaye mfanyakazi hupata stahiki zake kulingana na kima cha mshahara aliokuwa akiupata mpaka anapatwa na ugonjwa pamoja na kipindi alichochangia katika mfuko huo.

Kwa upande wa ajali na hasa tukijikita katika ajali za magari ni lazima kupata fomu ya Polisi namba 3, 90, 115 na ripoti kamili kutoka mfuko wa walipa fidia za wafanyakazi - WCF, kisha hujazwa. Kwa hiyo polisi ni lazima waandike ripoti, wapime hiyo ajali na kuelezea chanzo cha ajali, watu wa usalama kazini ni lazima pia wawe na maelezo yao katika ripoti yao, pia mtoa huduma ya afya lazima atoe ripoti ni kwa namna gani aliweza kumpokea majeruhi, huduma gani aliitoa na kumpeleka kwa gari za dharula ili akapatiwe matibabu mengine katika vituo vikubwa vya afya (kama ilihitajika)

Kampuni ya Yapi Merkezi imekuwa sikivu kwani haikuishia tu kutoa bima ya afya ya NHIF kwa wafanyakazi wake bali kila mwezi huchangia asilimia moja kwa kila mfanyakazi katika mfuko wa walipa fidia yaani WCF, hii imepelekea watu kupata stahiki zao kwa wakati pale wanapobainika kuwa na tatizo la kiafya linalotokana na kazi (ugonjwa au ajali au vyote).

Viongozi wa vyama vya wafanyakazi, idara ya rasilimali watu, idara ya afya na usalama mahala pa kazi na kamati ya afya na usalama kazini ni miongoni mwa idara/ vitengo vinavyotakiwa kuufahamu utaratibu huu, kwani wao ndio waelimishaji wakuu katika masuala yahusuyo haki na wajibu wa mfanyakazi katika masuala ya afya na usalama mahala pa kazi pamoja na masuala ya rasilimali watu.

Nazidi kusema kuwa sisi kama wahudumu wa afya wa kampuni ya Yapi Merkezi tupo vizuri kwani tunajitahidi kutoa elimu mara kwa mara kwa wafanyakazi wenzetu kuhusiana na mambo mbalimbali yahusuyo afya.

Mtaalamu wa afya katika maeneo ya kazi ni lazima kujua mambo makuu matatu nayo ni namna bora ya kutoa huduma ya afya ile ya dharula na kawaida ili kuhakikisha kila mfanyakazi anabaki kuwa na afya bora ya akili, mwili na kijamii wakati wote.

Pia ni lazima kushirikiana na watu wa usalama kazini hivyo tunawajibika vilivyo ili kuhakikisha mazingira ya kazi ya watu wetu yanakaguliwa na kuondolewa vitu vyote hatarishi. Mwisho tunapaswa kuzijua sheria zenye kuelezea haki za wafanyakazi (workers compensation act).

Sambamba na hayo yote tunawajibika kutoa elimu ya afya yenye kuwafanya wafanyakazi kuwa salama na uwezo wa kujikinga na maambukizi ya magonjwa ya mlipuko kama kifua kikuu, tauni na kipindupindu.

Tunapenda kutumia fursa hii kuwaambia wafanyakazi wenzetu juu ya kampeni ya ukimwi duniani ambayo kidunia hufanyika Desemba mosi na siku zinazoendelea, wajiandae maana tutawapatia elimu kwa kujikumbushia njia bora za kujikinga na maambukizi ya VVU/UKIMWI.

# NENO LA SHUKURANI KWA WADAU WA TRC NA WANANCHI KWA UJUMLA



*"Tunawashukuru kwa kutuunga mkono katika Miradi na Huduma zitolewazo na TRC, TRC inaendelea kuwashawishi wananchi kutumia huduma zetu na kushirikiana katika ulinzi wa miundombinu ya reli kwani reli hii ni ya watanzania, TRC tunajali na kuthamini mchango wenu"*

*Masanja Kungu Kadogosa*
*Mkurugeni Mkuu TRC*

Shirika la reli tanzania linatoa pongezi za dhati kwa rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuboresha miundombinu ya reli na kujenga reli ya kisasa na kimataifa kwani shirika limekuwa likishirikiana kwa hali na mali na serikali ya awamu ya tano pamoja na wadau mbalimbali kuhakikisha usafiri wa reli nchini unakua imara, bora na wa kisasa kwani kuiboresha miundombinu ya reli katika nchi ni hatua kubwa sana itakayopeleka nchi kufikia uchumi wa kati.

Wateja wa TRC wakiendelea kushirikiana na shirika na kuvumilia baadhi ya changamoto ikiwemo uboreshwaji wa njia za reli ambao hupelekea baadhi ya njia kufungwa, hivyo hatuna budi kutoa pongezi kwa wateja kwa kuonesha uzalendo wa hali ya juu na kuona umuhimu wa usafiri wa reli kwa kuendelea kutumia njia hiyo ya usafiri.

TRC imekua ikishirikiana na Mamlaka ya Bandari nchini katika kuhakikisha usafirishaji wa mizigo inayotoka nje ya Tanzania inasafirishwa kwenda maeneo ya Tanzania na nchi jirani ili kuepuka malalamiko na kuwa na uaminifu mkubwa kwa wateja wanaotoa mizigo yao bandarini kwa kutumia usafiri njia ya reli.

Shirika linatoa pongezi kwa wananchi kwa kuwa walinzi wa mali zao pamoja na kuitunza miundombinu ya reli, hakika mambo yanayofanywa na serikali ni kwa ajili ya umma yanapaswa kuungwa mkono hivyo ni jukumu letu wananchi kuwa walinzi wa kwanza ili nchi iweze kupata manufaa ya kile kinachofanywa na Serikali

Tunatumai TRC kupitia serikali ya awamu ya tano itaendelea kutoa huduma bora kwa wananchi na watumiaji usafiri wa reli , wa abiria na mizigo na kuzidi kuboresha miundombinu ya njia za reli haswa njia zilizokua zikitumika muda mrefu kuziboresha na kuweza mataluma mapya yenye kiwango cha juu ambapo itafanya treni kutembea kwa haraka zaidi ukilinganisha na mwanzoni.

Wananchi wakae tayari kutumia treni ya kisasa iendayo haraka, pindi tu awamu ya kwanza ya mradi wa SGR itakapokamilika, pia wananchi watapata fursa za ajira wakati ujenzi ukiwa unaendelea kwa awamu nyinginezo za mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa.

Lake Cement, Bakhresa Ltd, YARA Tanzania Ltd, Tanga Cement, Dangote Cement, Tanzania fertilizers, Tanzania Leaf Tobacco, World Food Program, Mohammed Enterprises, Mikoani Traders, Yapi Merkezi na China Civil Engineering Construction Corporation ni miongoni mwa makampuni ambayo ni wateja wakubwa wanaotumia usafiri wa njia ya reli, shirika linatanguliza shukrani za dhati kwa kuwa nasi kwa kipindi chote.

Rai yetu ni kuendelea kushirikiana kwa pamoja serikali pamoja na wadau wote wa reli wakiwamo wafanyabiashara, abiria na wananchi hasa wanaoishi pembezoni mwa reli.

Tunaahidi kuwa mtoa huduma bora zaidi na ya kuaminika ya usafiri wa reli Barani Afrika.



SHIRIKA LA RELI TANZANIA
Mtaa wa Reli/Barabara ya Sokoine
S.L.P 76959
Dar es Salaam
TANZANIA
Barua pepe; info@trc.co.tz
Tovuti; trc.co.tz
Simu ya Bure; 0800 110 042

Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
SHIRIKA LA RELI TANZANIA

| | |
|---|---|
| MHARIRI MKUU | Jamila Mbarouk |
| MHARIRI MSAIDIZI | Mohammed Mapondela |
| MTAYARISHAJI | Sami Omary |
| MAKALA | Aziza Charles |
| HABARI | Tracylinda Nganga |
| PICHA | Seleman Kadiko |
| KIBONZO | Hassan Said |

tzrailways TRC Reli TV

Reli Yetu | Maendeleo Yetu | Taifa Letu #TRCMpya